TAARIFA YA UPATIKANAJI WA HUDUMA YA MAJI HALMASHAURI YA WILAYA YA NGARA

1.0 MAJI VIJIJINI.

Halmashauri ya Wilaya ya Ngara imeendelea kutoa huduma ya maji kwa kutumia teknolojia mbalimbali kama vile maji ya bomba ya bubujiko, maji ya bomba ya kusukumwa na mitambo, chemichemi za asili zilizoboreshwa, visima vya pampu za mikono na uvunaji wa maji ya mvua.

Mtandao wa usambazaji maji safi na salama vijijini unakadiriwa kuwa **60.3%** hadi kufikia Mwezi Disemba 2018. Kiwango hiki cha mtandao kimezingatia upatikanaji wa maji salama bila kujali umbali unaotembewa na watumiaji. Hali halisi ya huduma ya maji Vijijini ni kama inavyooneka katika jedwali Na.**1** hapa chini.

Jedwali Na. 1: Upatikanaji wa Huduma ya Maji Vijijini Hadi Disemba, 2018

NA.	AINA YA MRADI	IDADI YA MIRADI ILIYOPO	MIRADI INAYOFANYA KAZI	WANAOPATA HUDUMA
1	Maji ya bomba bubujiko (gravity)	30	27	55,234
2	Maji ya bomba yanayosukumwa na mitambo	8	6	35,406
3	Vyanzo vya Maji vya asili vilivyoboreshwa	245	196	45,455
4	Visima vya pampu za mikono	270	198	36,300
5	Miradi ya uvunaji maji ya mvua	94	78	12,227
6	Maji ya bomba yanayosukumwa kwa nishati ya mionzi ya jua	2	2	8,371

1.1 TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA VIJIJI 10

Halmashauri ya Wilaya ya Ngara ni Miongoni mwa Halmashauri zinazotekeleza ujenzi wa miradi ya Vijiji 10. Katika Mwaka wa Fedha 2017/2018 Halmashauri ilipokea fedha Jumla ya Tsh. 314,314,716.05 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya Vijiji 10 ambapo Tsh. 235,268,101.05 ilikuwa ya kupeleka umeme kwenye miradi ya maji Kanazi/Kabalenzi, Muhweza/Murugarama na Mbuba. Tsh. 60, 896, 574 ni ya kulipa deni la Mkandarasi na Tsh. 18,150, 041 ni ya kulipa deni la Mhandisi Mshauri.

Kwa Mwaka wa fedha 2018/2019 hadi kufikia Mwezi Disemba, 2018 Halmashauri imeishapokea fedha ya utekelezaji wa miradi jumla ya Tsh. 167, 310,591 ambapo Tsh. 55,113,256 ni ya kulipa deni la Mkandarasi wa Mradi wa Muhweza/Murugarama, Tsh.103,953,617 ni ya kulipa deni la Mkandarasi wa Mradi wa Mbuba na Tsh.8,243,718 ni ya

kulipa deni la Mhandisi Mshauri. Bajeti ya Mwaka wa fedha 2018/2019 ni Tsh. 1,786,900,000. Orodha ya Miradi ya Maji chini ya programu ya Vijiji 10 ni kama inavyoonekana katika jedwali Na.2 hapa chini

Jedwali Na. 2: Orodha ya Miradi ya Maji chini ya programu ya Vijiji 10

Na.	Jina la Mradi	Wanu faika	Teknolojia	Gharama ya Mkataba	Kiasi kilicholipwa	Kiasi kilichobaki	Hali ya ya utekelezaji
1	Rulenge	8,378	Bubujiko (Gravity)	640,223,188	602,869,486	37,353,702.	100% na unatoa huduma
2	Ngundusi	3,994	Pampu ya umeme	345,745,446	341,745,446	4,000,000.00	100% na unatoa huduma
3	Mukibogoye	8,658	Pampu ya dizeli	240,659,633 .50	211,896,886	28,762,747.5	100% na unatoa huduma
4	Mukubu	6,291	Vyanzo vilivyobore shwa	102,795,000	63,764,000	39,031,000	100% na unatoa huduma. Upo kwenye muda wa matazamio
5	Munjebwe	4,456	Bubujiko	287,300,178	287,300,178	-	100%. Haujakabidhiwa kwa Wananchi kwasababu ya mapungufu yaliyojitokeza
6	Rwinyana	6,077	Bubujiko	501,192,260 .03	455,180,155	46,012,105.0 3	94% na unatoa huduma
7	Muruvyagira	5,721	Pampu ya umeme	254,694,632 .00	165,662,310	89,032,322.0 0	76% na hautoi huduma
8	Kanazi/Kabal enzi	8,476	Pampu ya umeme	498,189,626	272,223,760	225,965,866. 00	80% na hautoi huduma
9	Muhweza/Mu rugarama	7,986	Pampu ya umeme	559,209,132	245,349,631	313,859,501. 00	80% na hautoi huduma
10	Mbuba	7,111	Pampu ya umeme	524,652,382 .00	195,237,031	329,415,351. 00	75% na hautoi huduma
11.	Ununuzi wa mabomba ya Muhweza, Murugarama, Kanazi, Kabalenzi, Mbuba, Muruvyagira			852,430,000	700,993,000	151,437,000. 00	100%
12	Mhandisi Mshauri miradi ya Rwinyana, Mukibogoye na Munjebwe			99,700,000.	88,920,000.	10,780,000.	
13	Mhandisi			118,667,400	65,405,114.	53,262,286.0	

	Mshauri miradi ya Mbuba, Muhweza/Murugarama na Mukubu			.00	00	0	
14	Rulenge na Ngundusi			94,360,000.00	94,360,000.00	-	
15	Kanazi/Kabalenzi na Muruvyagira			75,263,290.00	52,199,621.25	23,063,668.75	
	Jumla			**5,195,082,167.53**	**3,843,106,618.25**	**1,351,975,549.28**	

1.2 MPANGO WA LIPA KWA MATOKE (PbR)

Halmashauri ya Wilaya ya Ngara ilikidhi vigezo na masharti ikafanikiwa kuingia kwenye Mpango wa Lipa kwa Matokeo unaofadhiliwa na DfID kwa Miaka yote miwili 2016/2017 na 2017/2018 ambapo kwa Mwaka 2016/2017 Halmashauri ilipokea fedha Tsh. 62,790,000 na Mwaka 2017/2018 ilipokelewa Ths. 69, 729,987.97. Halmashauri imetumia fedha hizi kufanya shughuli zifuatazo;

- Kukarabati Mradi wa maji Mugoma usiyofanya kazi kwa kununua transfoma ya umeme na kununua Mtambo wa kusukuma maji kwa kutumia nishati ya umeme. Transfoma na pampu vimeishafungwa. Tunawasubiri TANESCO waongeze nguvu ya umeme kwenye Transfoma ili Mtambo uanze kusukuma maji
- Kujenga chanzo cha maji Nyawhela kwa kushirikiana na Wananchi ili kupeleka huduma ya maji katika sekondari ya bweni ya Murusagamba. Shughuli hii imefanyika na maji yanafika shuleni.
- Kukarabati visima virefu na vifupi visivyofanya kazi. Utekelezaji wa shughuli hii unaendelea
- Kuchimba kisima ili kuongeza wingi wa maji katika mradi wa maji unaotumia nishati ya jua Kijiji cha Bukiriro. Utekelezaji wa Shughuli hii unaendelea.
- Kukarabati mradi wa maji Nterungwe. Utekelezaji wa shughuli hii unaendelea

1.3 MAFANIKIO

i) Katika miradi ya vijiji 10 chini ya programu ya WSDP Halmashauri ya Ngara tumefanikiwa kukabidhi miradi 3 kwa Wananchi. Miradi hiyo ni Rulenge, Ngundusi na Mukibogoye. Mradi wa maji Mukubu umekamilika upo kwenye kipindi cha matazamio. Munjebwe umekamilika ila bado haujakabidhiwa kwa Wananchi kwasababu ya mapungufu yaliyojitokeza. Mradi wa maji wa Rwinyana upo 94% na unatoa huduma kwa Wananchi.

ii) Tumepata fedha kutoka Wizara ya Maji za kupeleka umeme katika eneo la mitambo ya kusukuma maji ili kubadili teknolojia kutoka kwenye mitambo inayotumia dizeli kwenda kwenye mitambo inayotumia umeme ili kurahisisha uendeshaji wa miradi ya maji ya Kanazi/Kabalenzi, Muhweza/Murugarama na Mbuba.

iii) Kupata ufadhili wa ujenzi wa mradi mkubwa maji katika kijiji cha Rusumo, Ukarabati na upanuzi wa miradi katika Vijiji vinne vya Mshikamano, Kasharazi, Kasulo na Rwakalemera. Utekelezaji uko kwenye hatua ya kumpata Mhandisi Mshauri

atakayefanya shughuli ya usanifu. Miradi hii iko chini ya programu ya LADP (Local Area Development Program) inayofadhiliwa na Bank ya Dunia kupitia NELSAP.

1.4 CHANGAMOTO

i) Utekelezaji wa miradi unakwenda kwa kusuasua kutokana na Wakandarasi kukaa mda mrefu nje ya eneo la kazi kwasababu ya ukosefu wa fedha

ii) Kuchelewa kwa fedha za kulipa madai ya Wakandarasi. Madai ya Wakandarasi yaliyowasilishwa Wizara ya Maji ambayo fedha haijaletwa ni haya yafuatayo;

JINA LA MRADI	**MKANDARASI**	**KIASI**	**TAREHE YA KUWASILISHA**
Muruvyagira	Nyamasiriri Gen.Promo &Supplies Ltd	21,849,600.00	24/04/2018
Kanazi/Kabalenzi	Nyamasiriri Gen.Promo &Supplies Ltd	26,115,426.00	24/04/2018
Umeme Muruvyagira	TANESCO	143,911,301.16	24/04/2018
Mukubu	Rumanyika Investiment Co.Ltd	28,086,000.00	09/08/2018
Usimamizi miradi ya Muhweza/Murugarama, Mbuba na Mukubu	Engineering Research Associates Ltd	13,498,762.00	09/08/2018
JUMLA		**233,461,089.16**	

1.5 UTATUZI WA CHANGAMOTO

i) Halmashauri inaendelea kufuatilia fedha Wizara ya Maji ili kulipa madai ya Wakandarasi.

2.0 MAJI MJINI

Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji,

Mamlaka ya Maji Mjini Ngara ilitangazwa kwa **GN Na. 258** tarehe **21 Juni, 2002** na kuanza kazi rasmi tarehe **01 Julai, 2003**.

Chini ya sheria ya Maji na Usafi wa Mazingira **Na.12 ya mwaka 2009** Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Ngara Mjini (NGUWASA), imepewa jukumu la kusimamia na kutoa huduma endelevu ya maji na usafi wa mazingira katika mji wa Ngara chini ya usimamizi wa Bodi ya Maji. Bodi ya Sasa iliteuliwa 17 Novemba, 2017 na muda wake utaisha 30 Novemba, 2020. Mamlaka iko **kundi C** na **inalelewa na Halmashauri ya Wilaya ya Ngara**.

2.1 UZALISHAJI NA UTOAJI WA HUDUMA YA MAJI

Maji huzalishwa kwa kutumia **mitambo 3** inayotumia nishati ya umeme kutoka kwenye chanzo cha maji cha Mukidyama. Maji husambazwa kwa Wateja kwa njia 2 ambazo ni:-

(i) Kusukuma maji hadi kwenye matenki na baadae kuyasambaza kwa msereereko (***Gravity***) hadi kwa wateja na

(ii) Kusukuma maji moja kwa moja kutoka kwenye chanzo hadi kwa wateja bila kupitia kwenye matenki (***Direct pumping***)

MATENKI YANAYOTUMIKA [*UJAZO WAKE JUMLA NI 696M^3*]

NA	AINA YA TENKI	UJAZO WAKE	MAHALI LILIPO	ENEO LA HUDUMA	MAELEZO
01	TENKI LA MAWE	250M^3	NYAMIYAGA	Kanda ya Nyamiyaga na Mjini	Linahitaji ukarabati
02	TENKI LA MAWE	250M^3	KWA DC	Mjini	Linahitaji ukarabati
03	FERROCEMENT	46 M^3	IDARA YA MAJI	Ukanda wa Mzee Sebabili na Ujenzi	Ni zima
04	TENKI LA MAWE	75M^3	MUKIDIDILI	Mukididili/Mukirehe	Linahitaji ukarabati
05	TENKI LA CHUMA	75M^3	MURGWANZA	Murgwanza/ Mukanywampezi	Linahitaji ukarabati
	JUMLA	**696 M^3**			**Ujazo huu ni mdogo**

2.2 MAHITAJI YA MAJI KWA KULINGANISHA NA IDADI YA WAKAAZI WANAOISHI KWENYE ENEO LA MTANDAO WA MAJI, WANAOPATA HUDUMA YA MAJI NA JUMLA YA WATU WOTE

MWAKA	MAHITAJI YA MAJI KWA DISEMBA [M^3]	MAJI YALIZOLISHWA DISEMBA 2018 [M^3]	JUMLA YA WATU	WANAOISHI KWENYE ENEO LA MTANDAO	%	WANAOPATA HUDUMA YA MAJI	%	JUMLA YA MITA ZA MAJI [CONNECTIONS]
2017/18	**75,000**	**32,620**	**35,669**	**23,212**	**65**	**22,481**	**63**	**2,713**

2.3 AINA YA WATEJA NA IDADI HADI DISEMBA, 2018

Na	KUNDI	IDADI
01	Watumiaji maji majumbani [Domestic]	2477
02	Taasisi mbali mbali [Institutions]	115
03	Maeneo ya biashara [Commercial]	91
04	Vilula [Viosks]	30
	JUMLA	**2,713**

2.4 HALI YA HUDUMA

NGUWASA ina lengo mahsusi la kutoa huduma ya maji kila siku kwa wakazi wa mji wa Ngara kwa kutumia teknolojia ya mitambo 3 ya kusukuma maji kutoka kwenye chanzo cha maji chini ya ardhi. Katika kipindi cha Disemba, 2018 hali ya upatikanaji wa maji katika maeneo mengi ya mji wa Ngara:- Mubinyange, Nyamiaga, Murgwanza, Nakatunga na Buhororo siyo ya kuridhisha kutokana na umeme kutokuwa na nguvu ya kutosha kuendesha mitambo ya kusukuma maji pamoja na kuharibika kwa kifaa (bush) katika mtambo mmoja wa kusukuma maji kulikopelekea kusambaza maji kwa kutumia mitambo miwili badala ya mitambo mitatu.

2.5 WATEJA

Katika kipindi cha kufikia 31 Disemba, 2018 Mamlaka ina jumla ya wateja 2,713

2.6 MCHANGANUO WA MAPATO NA MATUMIZI KWA KIPINDI CHA DISEMBA, 2018

2.6.1 MAPATO: Mapato ya Mwezi Disemba, 2018 ni jumla ya Tsh. **9,046,965.00**

2.6.2 MATUMIZI: Jumla ya matumizi kwa kipindi cha Disemba, 2018 ni Tsh. **9,640,520.00**

2.7 MADENI MWAKA 2018/2019

Hadi kufikia tarehe 31 Disemba, 2018, madeni makubwa kutokana na mauzo ya maji ni kiasi cha **Tzs. 18,986,400.00 .** Sehemu kubwa ya deni hilo linatokana na baadhi ya taasisi za Serikali:- Magereza **Tzs. 14,996,840,** Taasisi nyinginezo **Tzs. 2,726,400.00** na watumiaji wa kawaida wa majumbani **Tzs. 1,263,160.00**

2.8 CHANGAMOTO/UFUMBUZI/MAOMBI MAALUM

2.8.1 CHANGAMOTO AMBAZO MAMLAKA IMEKABILIANA NAZO

- Muda mwingi umeme kuwa na nguvu ndogo chini ya Voliteji 380 inayopelekea kushindwa kuendesha mitambo ya kusukuma maji. Pia umeme unakatika mara kwa mara kwa muda mrefu. Hii huathiri zoezi la kupeleka huduma ya maji kwa Wateja.
- Mahitaji makubwa ya maji kulinganisha na uzalishaji halisi wa maji. Mahitaji kwa siku ni mita za ujazo 2,500 na uzalishaji wa maji ni wastani wa mita za ujazo 1,500 kwa siku. Hii husababisha maji kutolewa kwa mgao ambapo maeneo mengine yanapata maji mara moja kwa wiki.
- Uchakavu wa miundombinu ya maji unaopelekea NRW (upotevu wa maji) kuwa 48%
- Baadhi ya ya wateja binafsi pamoja na taasisi za Serikali kushindwa kulipia maji kwa wakati.
- Kupanda kwa gharama ya umeme wa kuendeshea mitambo ya kusukuma maji na kusababisha Mamlaka ishindwe kutekeleza majukumu yake mengine, kwa mwezi mmoja gharama za ankra za umeme zinafikia wastani wa Tzs. 12,000,000.00
- Mradi kutofanyiwa ukarabati na ujenzi mkubwa kutokana na kutokuwa na fedha za kutosheleza mahitaji halisi.

2.8.2 MBINU ZA KUKABILIANA NA CHANGAMOTO ZILIZOPO

- Mamlaka ya Maji inaendelea kufanya ufuatiliaji TANESCO juu ya utatuzi wa suala la umeme kutokuwa na nguvu za kuendesha mitambo ya maji.
- Mamlaka ya Maji imewasilisha ombi la fedha Tsh. 399,937,650 Wizara ya Maji ili kuchimba kisima kikubwa chenye kipenyo cha inch 10 na kufunga pampu kubwa inayozalisha maji mita za ujazo 80 kwa saa ili kuongeza uzalishaji wa maji utakaopunguza kero ya upatikanaji wa maji katika mji wa Ngara kwa matokeo ya muda mfupi wakati tukisubiri ujenzi wa mradi mkubwa wa maji kupitia Mamlaka ya Maji Bukoba (BUWASA).
- Kufanya matengenezo endelevu ya mara kwa mara ya mfumo wa mabomba ili kudhibiti mivujo
- Kuchukua hatua za kisheria dhidi ya wateja wanaoshindwa kulipia kwa wakati ankra zao za maji. Pia Barua mbali mbali zimekuwa zikiandikwa kukumbushia ulipaji wa madeni husika kwa Taasisi.
- Mamlaka imefanya mchakato wa kufanya mabadiliko ya bei ya mauzo ya maji ili iweze kumudu kununua umeme na kuweza kutekeleza majukumu mengine. Mamlaka ya Udhibiti wa Nishati na Maji (EWURA) imeidhinisha mabadiliko ya bei mpya ya mauzo ya maji kupitia Gazeti la Serikali Na.803 la tarehe 28/12/2018.

Nawasilisha.

Aidan J. Bahama
MKURUGENZI MTENDAJI,
HALMASHAURI YA WILAYA YA NGARA